# Hogweed Kubwa

*Heracleum mantegazzianum* **Familia ya Dania**

**Aina A Kwekwe Hatari: Inahitaji Kuangamizwa**

## Namna za Kutambua

- Mmea mkubwa wa kichwa cha maua cha upana wa futi 2, mfano wa mwavuli wenye mashada ya maua yaliyojaa maua madogo
- Hufikia urefu wa futi 8 hadi15 ikiwa kwenye maua
- Mashina ya mrija, yenye mistari, upana wa inchi 2 hadi 4 ina madoa ya kuenuka mekundu-zambarau na nywele nyeupe ngumu (inafanana na miiba lakini ni nywele)
- Majani makubwa ya kuenea na mistaki ya kina, upana wa futi 3 hadi 5
- Sehemu za chini za majani zina nywele kwenye mbavu lakini uso wa sehemu ya chini ya jani haina nywele
- Ukubwa wa mbegu ni inchi 3/8, matunda mviringo tena makavu yenye mabawa na mikondo iliyovimba ya rangi ya kahawa



*Tafuta maua meupe makubwa, ya mfano wa mwavuli kuanzia katikati ya Mei na Julai.*

## Biolojia

Kawaida mmea huu ni wa kudumu (perennial), huota maua mwakwa wa 3 au baadaye na kawaida hufa baada ya kuota maua. Mbegu zenye mabawa husambaa kwa maji, kusonga kwa udongo au na wanyama; zinaweza kudumu katika udongo kwa miaka 10. Mimea huanza kuchomoza mapema msimu wa masika (spring). Maua katikati Mei hadi Julai, mbegu huanza kutokea Julai.



*Shina zina rangi nyekundu-zambarau na madoa yakuenuka na nywele nyeupe.*

## Matokeo

**Ni sumu. Majimaji yanaweza kusababisha malengelenge ya ngozi na kovu za daima.** Hubana nyasi asilia na mimea ya chakula inayopendwa kwa sababu humea kwa mabavu. Huenda ikazidisha mmomonyoko kwenye mito na maeneo ya milima kuwa kubadilisha nyasi zinazolinda udongo na mimea ya mbao.

## Kuenea

Asilia yake inatoka Milima ya Caucasus na ililetwa Amerika ya Kaskazini kama mmea wa mapambo. Kawaida hupatikana sana maeneo ya mji, ukingo wa barabara, viwanja visivyotunzwa na vile visivyotumiwa. Hupendelea udongo wa rotuba, usio mkavu na inaweza kukua kwenye hali mbalimbali za mwangaza. Kwa kuwa huzaa mbegu kwa wingi ajabu na inastahamili kivuli, kwa upesi sana inaweza kuvamia ukingo wa mto na mkondo wa maji, chemichemi za maji na mabonde yenye miti.



*Majani ni makubwa sana yenye mistari mizito.*

## Unachoweza Kufanya

Programu ya King County ya Kudhibiti Kwekwe Hatari (King County Noxious Weed Control Program) inaendeleza bidii kubwa ya kuangamiza hogweed kubwa maeneo yote ya kaunti. Changia juhudi zako kwa kukagua kuweko kwa hogweed kwenye mali yako. Kwa kuzuia uzalishaji wa mbegu na kuangamiza mimea kuliyoko, itapunguza kuenea kwake au itaangamizwa baada ya mda. Kama huwezi kudhibiti hogweed kubwa yako, wasiliana nasi upate usaidizi. Tafadhali piga ripoti unapoiona.

## Namna ya Kudhibiti

Ukipata hogweed kubwa kwako, chagua moja au mchanganyiko wa namna za kudhibiti zilizotajwa hapa chini. Fanya makini **Mmea huu ni hatari kubwa kwa afya.** Vaa nguo imara, viatu, na miwani unapojaribu namna zozote za kudhibiti. **Epuka kugusa kwa ngozi. Majimaji kwenye majani na shina inaweza kusababisha kuungua, malengelenge na makovu.**

### *Kutumia Mikono:*

Mimea iliyokomaa inaweza kuondolewa kwa mikono. Chimba angalau inchi 4-6 ya mzizi mkuu. Mimea michanga ni sugu zaidi. Kwa iliyokomaa, miche midogo inaweza kukua kwa mamia kadhaa na inaweza kuvunjika inapong'olewa kwenye udongo ulioshikana, ikaacha mizizi iendelee kukua. Hakikisha unatia maua na miche midogo kwenye mifuko ya karatasi na utupe kwenye takataka.

### *Kutumia Mashini:*

Kukata kwa mashini sio namna thabiti ya kudhibiti kwa mda mrefu. Usikate kwekwe kwa panga wala mashini bila viatu na nguo imara za kulinda mwili—majimaji kutoka kwa mimea inaweza kuchoma mwili.



*Tahadhari: majimaji ya mashina yanaweza kusababisha malengelenge na makovu makali sana.*

### *Dawa za Kemikali:*

**Zingatia sheria na masharti yote yanayostahili kuhusu matumizi ya dawa ya kuuwa kwekwe (herbicide) hapo kwako, na ufuate maelezo yote ya kibandiko (label).** Glyphosate ni imara, lakini ni dawa ya kuuwa kwekwe isiyochagua (non-selective) ambayo pia huuwa nyasi sehemu inayopulizwa. Sehemu bila mimea zinaweza kuvamiwa tena kwa hivyo, panda upya mimea inayostahili sehemu hiyo. Triclopyr ni imara pia. Ni dawa ya kuuwa kwekwe inayochagua (selective) inayoangamiza tu mimea ya majani mapana, bila kuumiza aina nyingi ya nyasi. Eneza dawa ya kuuwa kwekwe kwenye sehemu zote za majani na mashina ya mimea inayoendelea kukuwa; usikate shina baada ya kutumia dawa kwani itazuia mmea kunyonya dawa. Sehemu iliyovamiwa na miche mingi inaweza kudhibitiwa vyema kwa kutumia dawa ya kuuwa kwekwe msimu wa masika (spring), na ikiwezekana itumiwe tena msimu wa kiangazi kwa zile zinazomea kuchelewa. Kwa maelezo zaidi, wasiliana na Programu ya Kudhibiti Kwekwe Sumu (Noxious Weed Control Program).

# Inaweza kufananishwa na:

**Hogweed kubwa wakati mwingine inaweza kufananishwa na mmea asilia cow parsnip (*Heracleum maximum*), pamoja na aina ya karoti mwitu iliyoletwa (*Daucus carota*) na hemlock-sumu (*Conium maculatum*).**



*Cow parsnip inafanana sana na hogweed kubwa lakini kawaida ina urefu wa futi 4-7, na ina mafungu ya maua madogo tena laini,nywele za kung'ara, ikiwa ni pamoja na kwenye sura ya chini ya majani. Pia, mbegu zake zina umbo la moyo. Kama hogweed, inaweza kusababisha kuchomeka, kwa hivyo* **epuka kugusana na majimaji.**



*Karoti mwitu maua yake hufanana na yale ya hogweed kubwa, lakini mmea huu hufikia urefu wa futi 3 pekee.*



*Hemlock-sumu inaweza kutofautishwa na hogweed kubwa kwa shina zake zisizokuwa na nywele na mafungu yake mengi tena madogo zaidi kwa kila mmea.*

**Swahili**
Juni 18:

**206-477-WEED (206-477-9333) or TTY: 711**
**kingcounty.gov/weeds** **noxious.weeds@kingcounty.gov**

King County

"cow parsnip Heracleum maximum" ya Paul Asman na Jill Lenoble / CC BY 2.0.
"Daucus carota" ya Andreas Rockstein / CC BY 2.0.
Faili: NoxWfact-Giant-Hogweed-2018.indd